



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UAMUZI WA RUFAA ZA
WAGOMBEA UDIWANI

Dar es Salaam, 14 Septemba, 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha tarehe 13 Septemba 2020 imepitia, imechambua na kuzifanyia uamuzi rufaa za wagombea Udiwani zilizowasilishwa na wagombea kupitia kwa Wasimamizi mbalimbali wa Uchaguzi nchi nzima.

Rufaa hizo zimewasilishwa chini ya kifungu cha 44 (5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ambacho kinatoa fursa kwa wagombea wa Udiwani kukata rufaa wanapokuwa hawajaridhika na uamuzi wa Wasimamizi wa Uchaguzi kutokana na pingamizi zilizowasilishwa.

Aidha, chini ya kanuni ya kanuni ya 30 (3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Madiwani) za mwaka 2020, Tume inaweza kukubali au kukataa rufaa hizo.

Katika kikao hicho, Tume imezipitia, kuchambua na kuzifanyia uamuzi jumla ya rufaa 49 za Wagombea Udiwani, kama ifuatavyo:-

- i. Imekubali rufaa **24** na kuwarejesha wagombea Udiwani katika orodha ya wagombea Udiwani. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Kata za Mlangarini (Arumeru Magharibi), Nduruma (Arumeru Magharibi), Nkungulu (Magu), Ibungilo (Ilemela), Itumbili (Magu), Mlandege (Iringa Mjini), Mdoe (Handeni Mjini), Sinza (Ubungo), Kisongo (Arumeru Magharibi) Uhuru (Dodoma Mjini), Bunju (Kawe), Kwa Kilosa (Iringa Mjini), Kimbiji (Kigamboni), Msambweni (Tanga Mjini), Nsalala (Mbeya Vijijini), Nzuguni (Dodoma Mjini), Madukani (Dodoma Mjini), Kerege (Bagamoyo), Kibaoni (Kilombero), Kolo (Kondoa Mjini), Lumemo (Kilombero), Melela (Mvomero) na rufaa mbili za Kata ya Moivo (Arumeru Magharibi).
- ii. Imekataa rufaa **19** za wagombea Udiwani ambao hawakuteuliwa. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Kata za Duru (Babati Vijijini), Nundu (Nyang'hwale), Magugu (Babati Vijijini), Sangamwalugesha (Maswa Mashariki), Pongwe (Tanga Mjini), Mpandangindo (Peramiho), Mji Mwema (Kigamboni), Kinampanda (Iramba Magharibi), Mbelekeshe (Iramba Magharibi), Maendeleo (Mbeya Vijijini), Nalasi Mashariki (Tunduru Kusini), Nyakabindi (Bariadi), Nzovwe (Mbeya Mjini), Ndulungu (Iramba Magharibi), Kwediyamba (Handeni Mjini), Kyengege (Iramba Magharibi), Kisiriri (Iramba Magharibi), Maluga (Iramba Magharibi) na Ndago (Iramba Magharibi)
- iii. Imekataa rufaa **6** za kupinga wagombea Udiwani walioteuliwa. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Kata za Kisanga (Kalambo),

Mwigobero (Musoma Mjini), Kirima (Moshi Vijijini), Gangilonga (Iringa Mjini), Majengo (Mbeya Mjini) na Lipangalala (Kilombero).

Idadi hii inafanya jumla ya rufaa za wagombea Udiwani zilizotolewa uamuzi kufikia **244**. Tume itaendelea kutoa matokeo baada ya usajili na uchambuzi wa rufaa hizo kila siku. Wahusika wa rufaa hizo watajulishwa kwa barua juu ya uamuzi wa Tume.



Dkt. Wilson Mahera Charles

MKURUGENZI WA UCHAGUZI
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI